

Hakika twahuzunika

1. Mechi nyingi ni huzuni, wenzenu twahuzunika
Mchezapo uwanjani, mnatutia mashaka
Magoli yatinga ndani, bila hata ya mipaka
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
2. Msidhanie utani, wapenzi twasononeka
Mlipokwenda Benini, manne walisondeka
Wakenya hapa nyumbani, matano walibandika
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
3. Ikaingia Sudani, nchini ilipofika
Bila ugumu nadhani, mawili yalitingika
Yaliingia nyavuni, butwaa ilitushika
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
4. Mngali usingizini?, wanazi tulishamaka!
Ugenini na nyumbani, kote kote ni mashaka
Mwingiapo uwanjani, nyuso zetu twafunika
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
5. Katikati uwanjani, mpira hupendezeka
Uelekee golini, huzuni huongezeka
Twaingia mashakani, twajua mtapitika
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
6. *Stars* naamini, mwaweza kutofungika
Mchezapo kwa makini, ni nani wakupitika?
Muwekapo madhumuni, kwa timu nzima husika
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
7. Chenga zilizo laini, mwaweza bila kuchoka
Msizubae njiani, mwendako mtajafika
Mtatingisha nyavuni, mpira mtauweka
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
8. Msifungwe kilaini, ni lini mtashituka?
Mshupae misulini, mlima usopandika!
Dhamira yangu makini, wasiwaone vichaka
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
9. Utadhani guniani, nyavuni wakipachika
Twaulizana vichwani, iweje mlishachoka?
Twabakia na huzuni, ni lini tutaja cheka?
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
10. Kwenu miye si mtani, hakika tunakereka
Uzalendo u damuni, wazawa twakasirika
Tujefanya kitu gani, muweze ngangarika?
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
11. Tanzania masikini, mabao yanatingika
Hata vinchi laini, magoli vyatubandika
Nako FAT kulikoni, siwaoni kung'atuka!
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
12. Mpira wenu si duni, hapa kwetu Afrika
Tatizo li miguuni, yenu kwenu kukunjika
Na ustadi golini, kujua pa kupindika
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
13. Pia huko zoezini, siyo pa kuvinjarika
Timu ni kama kundini, pamoja kuchakarika
Mpatiane maoni, lengo kuu ushirika
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
14. Muendapo ziarani, twadhani mwanunulika
Hatupati burudani, mbali ya kukashifika
Hata muwapo nchini, twawahisi vibaraka
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
15. Arusha mashindanoni, kweli tulikung'utika
Mawili ndiyo mwanzoni, Uganda kutubandika
Iweje ni ushindani, kila siku twafungika?
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
16. Tulidhani burudani, dimba lilipofunguka
Bonde mteremkoni, kombe lilituonyoka
Kulitia mikononi, mabingwa walisifika!
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
17. Mijini na vijijini, sababu tusha zichoka
Twashangaa kuna nini, kila leo twafungika
Tumechoshwa mkiani, kila siku kuushika!
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!
18. Ninafika kituoni, hasira zinanishika
Waungwana fikirini, tumegeuzwa vichaka
Hamsa wa ishirini, sababu waziandika!
Hakika twahuzunika, mcharazwapo mabao!

Msanif Shaaban
SLP 2180335
Dar Es Salaam
Tanzania